

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA MARA:

Simu Na.028 2621055

Nukushi .Na.0282621264

Barua pepe: ded@bundadc.go.tz

Tovuti www.bundadc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P 126,

BUNDA.

02/03/2022

**YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MUDA YA KUKUSANYA TAARIFA ZA
ANUANI ZA MAKAZI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA.**

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA
ANAPENDA KUWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA NAFASI ZA
AJIRA YA MUDA YA KUKUSANYA TAARIFA KWENYE ZOEZI LA ANUANI ZA
MAKAZI KATIKA VITONGOJI 388 VILIVYOPO KATIKA HALMASHAURI YA
WILAYA YA BUNDA.

1.0SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 40
- Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda
- Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- Awe anamiliki simu janja (smartphone) inayoweza kukaa na chaji kwa muda mrefu
- Awe na barua pepe inayofanya kazi
- Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri ramani za vijiji na vitongoji
- Awe anaishi kata anayoomba kufanyia kazi
- Awe mwaminifu na mwadilifu na anaefanya kazi kwa kujituma

2.0 MAJUKUMU

- Kugawa na kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwenye vitongoji
- Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja, maeneo ya kutolea huduma za jamiii na biashara kwenye vitongoji kwa kutumia mfumo wa anauani za makazi
- Kutuma taarifa (data) kwenye mfumo wa anauani za makazi kila siku
- Muda wa kazi utazingatiwa kwenye mkataba wa kazi ya muda.

3.0 MAOMBI YA AJIRA YA AMBATISHWE

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA
- Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- Picha mbili passport size za sasa (moja ibandikwe kwenye barua ya maombi nyingine iambatishwe kwenye barua)

4.0 MALIPO

- Kiwango cha malipo kitaainishwa kwenye mkataba wa ajira ya muda

5.0 JINSI YA KUTUMA MAOMBI

- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anuani kamili ya muombaji, barua pepe (email) na kata anayotoka, barua zote zipitishwe na mtendaji wa kijiji au kata anayotoka

Barua zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwa anuani ifuatayo :-

Mkurugenzi mtendaji (W)

Halmashauri ya wilaya ya bunda


S.L.P 126

Bunda

Na kuzipeleka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) iliyopo katika kata ya kibara.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYA NI TAREHE 06/03/2022 SAA 09:30 ALASIRI

Tangazo limetolewa na



**Changwa M. Mkwazu
Mkurugenzi mtendaji (W)
Halmashauri ya wilaya
BUNDA.**